

For More Free KCSE Past papers visit [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)

102/3  
KISWAHILI  
Karatasi ya 3  
FASIHI  
MACHI/APRIL 2013  
Muda. Saa  $2\frac{1}{2}$   
Kidato cha 4

## MTIHANI WA MWIGO WA SHULE ZA WILAYA YA ELDORET MASHARIKI - 2013

(Hati ya kuhitimu Kisomo cha Sekondari)

Kiswahili

Karatasi ya 3

### MAAGIZO

- Jibu maswali manne pekee.
- Swali la Kwanza ni la lazima
- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki.
- Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

## **1. FASIHI SIMULIZI (LAZIMA)**

Eleza maana ya maneno haya

- a) Soga (alama 2)
- b) Miviga (alama 2)
- c) Eleza umuhimu wa magham (alama 6)
- d) Taja methali zenyе maana sawa na hizi. (alama 3)
  - i) Jifya mojo haliinjiki chungu
  - ii) Mavijya kale hayaachi kunuka
  - iii) Jikiona vyaelea vimeundwa
- e) Eleza sifa za misimu. (alama 7)

## **SHAIRI**

**Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata**

### **Bahari**

1. Bahari uzuri, wake tawambia  
Sifa tabashiri, kuwahadithia  
Ambazo ni nzuri, na faida pia.
2. Na faida pia, na kwamba ujue,  
Nakukuelela, nawe utambue  
Na sasa sikia, uzifafanue.
3. Uzifafanue, bahari za pambo  
Lenye uzuriwe, pia na urembo  
Ni siri ujue, na pia ni tambo.
4. Na pia ni tambo, ni siri yakini,  
Aidha ni fumbo haiwezekani,  
Ina mengi mambo, yenye na thamani.
5. Na pia ni thamani, kwa watu wa pwani,  
Nawapa yakini, nanyi sikizani,  
Humo baharini, kwanza pulikani.

6. Kwanza pulikani, lulu twaipata,  
Samaki yakini, faida huleta,  
Aidha wendani, pia huokota.
7. Pia huokota, ambari zinduma,  
Munyu na mafuta, vinapatikana,  
Faida yaleta, pulikiza sana.
8. Pulikiza sana, tia sikioni,  
*Tijaya* maana ilo baharini,  
Inapatikana, kwa kila ya fani.
9. Kwa kila ya fani, samaki twauza,  
Mapezi yakini, ya papa sikiza,  
Huleta thamani, yenye muangaza.
10. Yenye muangaza, pia na forodha,  
Pato huongeza, la kuleta fedha,  
Pia yaangaza, bahari kwa adha.
11. *Bahari kwa adha, adhaye* upepo,  
Hapana orodha, na ichafukapo,  
Huondoka ladha, tena hapo ndipo.
12. Tena hapo ndipo, chombo hutotoma,  
nyote muliopo, hapana msema,  
Ndipo muliyapo, “mama yoo mama!”

### Maswali

- a) Shairi hili ni la bahari gani? Eleza sababu yako. (alama 3)
- b) Taja faida mbili na hasara mbili za bahari kama anavyoeleza mshairi. (alama 4)
- c) Kwa kuzingatia beti mbili za mwisho, eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
- d) Kwa kutoa mifano, eleza idhini za kishairi alizotumia mtunzi. (alama 4)
- e) Andika ubeti wa nane katika lugha nathari. (alama 3)

- f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yaliyotumika katika shairi. (alama 2)
- i) pulikani
- ii) adhaye

**RIWAYA S. A. Mohamed: Utengano**

**Jibu swali la 3 au 4**

3. Unafiki unajitokeza waziwazi katika riwaya ya Utengano; Fafanua. (alama 20)
4. “come on...” sasa kwa upole huku akiyumbayumba. “Nini bwana?”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Eleza sifa zozote tatu za msemewa. (alama 6)
- c) Fafanua masaibu yaliyompata msemewa katika maisha yake. (alama 10)

**TAMTHILIA Mstahiki Meya**

5. “Sisi wafanyikazi tuna matatizo mengi yaliyotuzonga kwa muda mrefu. Kwanza mishahara yetu ni midogo”
- a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Kauli hii ilitolewa na nani? (alama 2)
- c) Taja na ueleze kwa kifupi matatizo mengine yaliyokabili jamii inayosawiriwa katika diwani hii. (alama 8)
- d) Utatuzi wake ulikuaje? (alama 6)
6. Jadili jinsi maudhui ya usaliti yanavyofafanuliwa katika tamthilia ya Mstahiki Meya. (alama 20)

**Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine; Ken Walibora na Said A. Mohammed.**

7. “Tusije tukajadili kuhusu ulevi wangu daima katika nyumba hii”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Fafanua sifa za mzungumzaji wa maneno haya. (alama 8)
- c) Taja na ueleze madhara ya ulevi ukirejelea hadithi inayozungumziwa. (alama 8)
8. Jadili maudhui ya ubaguzi na unyanyasaji kama yanavyojitokeza katika hadithi ya Damu Nyeusi - Ken Walibora (alama 20)